

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

Anuani ya Simu: "TAMISEMI"  
Simu Na: (026) 2322848, 2321607  
2322853, 2322420  
Nukushi: (026) 2322116, 2322146  
2321013  
Barua pepe: [ps@tamisemi.go.tz](mailto:ps@tamisemi.go.tz)



Tawala za Mikoa na  
Serikali za Mitaa,  
S.L.P. 1923,  
DODOMA.

**TAARIFA KWA UMMA.**

**MAELEZO YA KUELIMISHA UMMA JUU YA UCHANGIAJI WA  
ELIMU UNAOFANYWA NA WANANCHI.**

**1.0. UTANGULIZI**

Serikali ya awamu ya tano chini ya Uongozi wa Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli kuanzia mwezi Januari, 2016 imeanza kutoa elimumsingi bila malipo kama ilivyoainishwa katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na Ibara ya 52 (a) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi katika kampeni zake kwa wananchi kwa ajli ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015.

Tayari Serikali imetoa Waraka wa Elimu Namba 6 wa Mwaka 2015 unaofafanua na kubainisha majukumu ya serikali na wadau mbalimbali katika utekelezaji wa elimu msingi bila malipo.

**2.0. HALI YA UANDIKISHAJI**

Hadi kufika mwishoni mwa mwezi Januari, 2016 Jumla ya wanafunzi 9,771,902 kati yao 8,301,759 wa elimu ya msingi na 1,470,143 wa sekondari wanapatiwa na serikali elimumsingi bila malipo kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne.

### **3.0. UCHANGIAJI WA HIYARI WA WAZAZI/WALEZI**

Tukumbuke kwamba azma ya serikali ya kutoa elimumsingi bila malipo haizuii wadau mbalimbali wa elimu kuchangia maendeleo ya elimu kwa hiari. Wadau wakiamua kuchangia kwa nia ya kushughulikia kero fulani iliyopo katika shule yao au shule zao baada ya kupata kibali wanaruhusiwa kufanya hivyo.

Hapa napenda kufafanua kwamba wakati zoezi hili linaanza kibali cha uchangiaji wa elimu msingi bila malipo lilikuwa linatolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-TAMISEMI pekee kwa lengo la kudhibiti michango holela.

Kwakuwa hali imekuwa nzuri hivi sasa ukilinganisha na wakati zoezi hili lilipokuwa linaanza kutokana na uelewa wa dhana nzima ya utoaji elimu bila malipo kuongezeka, sasa Wakuu wa Mikoa wanaruhusiwa kutoa vibali hivyo baada ya kujiridhisha kuwa taratibu zilizowekwa zimefuatwa kikamilifu.

### **4.0. HITIMISHO**

Dhana ya utekelezaji wa utoaji wa elimumsingi bila malipo ni vema ikaeleweka vizuri kwa viongozi watakaohusika katika kusimamia utekelezaji wake. Vile vile wazazi au walezi, kamati na Bodi ya Shule pamoja na jamii wanalo jukumu la kuelewa majukumu yao ipasavyo.

Juhudi za makusudi zinapaswa kufanywa na viongozi na watendaji wa elimu ili kuwezesha jamii kufahamu wajibu wao katika utekelezaji wa elimumsingi bila malipo na hatimaye kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

**Imetolewa na:**

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Ofisi ya Rais-TAMISEMI

03/03/2016